# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


Namba ya shule **S0228**

Namba ya mtihani **S0448**

Mkuu wa Shule

**0767178869/0716103839**

Makamu Mkuu wa Shule **0755872859/0673872859**

Matron/Patron **0656545080**

**Shule ya Sekondari SADANI**

**S.L.P 284**


**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SADANI HALMASHAURI YA MUFINDI MKOA IRINGA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **Sadani** ipo umbali wa Kilometa **40** Magharibi mwa Mji wa **Mafinga** Usafiri wa basi kutoka mjini **Mafinga** unapatikana katika kituo cha mabasi **Kinyanambo A** (**Standi mpya**) Nauli ni Shilingi 4000 kwa basi na Shilingi **5000** kwa noa.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suti rangi nyeusi, suruali zishonwe vizuri na ziwe na marinda mawili na zisiwe nyembamba chini (**pima inchi 16-18**).
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni track nyeusi yenye mistari myeupe aina ya adidas, tishirt ya kijivu isiyokuwa na kola pamoja raba nyeusi.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Nguo za kushindia ni suruali mbili nyeusi na tishirt ya blue (unaweza kuipata Jirani na shuleni kwa Tsh 13,000/=)
viii. Tai mbili nyeusi

NB: **Huruhusiwi kuja na nguo nyingine yeyote isiyo sare ya shule. Hivyo mwanafunzi anapaswa kuripoti akiwa amevaa track nyeusi au sare ya shule.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo anayosoma.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi nne (4) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika .
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;

vi. Godoro futi mbili na nusu
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink/blue bahari, blanket 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2, 1 ndogo (lita Kumi),1 kubwa(lita ishirini) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini, reki yenye mpini 1, mifagio 2 (chelewa 1, soft broom 1) pamoja na mopa.
xii. Tochi 1/solata1
xiii. Sanduku linalofunga vizuri kwajili ya kuhifadhi vitu vyako.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Result slip

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule PRIVATUS HAULE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0767178869/0716103839.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755872859/0673872859**
- **Mwandamizi Taaluma0766633879/0713694887**
- **Mwandamizi Malezi 0762047656/0620832656**

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

**A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE**

i. Jina la mwanafunzi..........................................................................................................
ii.Tarehe ya kuzaliwa...................................mahali..........................................................
iii.Jina la baba............................................yu hai/amefariki.............................................
iv. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji..............................kata............................tarafa............................................
v. Kazi ya baba.....................................................................................................................
vi. Anwani yake............................................................simu...........................................
vii. Jina la mama.......................................yu hai/amefariki...............................................
viii. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji............................kata.............................tarafa............................................
ix. Kazi ya mama.................................................................................................................
x. Anwani yake................................................................simu.......................................
xi. Jina la mlezi....................................................................................................................
xii. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji.............................kata...........................tarafa.............................................
xiii. Anwani yake...........................................................simu..........................................

**B. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

| **NA** | **JINA** | **UHUSIANO** | **NA.YA SIMU/ANWANI** |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

**C. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE(MWANAFUNZI)**

Mimi.................................................naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule.Sitajihusisha na migomo,fujo wala makosa ya jinai.

Sahihi........................................tarehe..............................................

**D. AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi....................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu,naahidi kumpatia ada ya shule,michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Sahihi........................................tarehe..................................................

**PRESDENT OFFICE-REGION ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MUFINDI DISTRICT COUNCIL**
**SADANI SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognize Hospital in respect of all new entrants to Sadani Secondary School.

Full name..............................................................................
Age...........................................................

1. Blood comment (Red&White)..........................................................................................
2. Urine examination.....................................................................................................
3. Stool examination.....................................................................................................
4. Syphilis test..............................................................................................................
5. T.B test.....................................................................................................................
6. Ear test.....................................................................................................................
7. Eye test.....................................................................................................................
8. Spleen.........................................................................................................................
9. Abdominal...................................................................................................................
10. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease:
    .........................................................................................................................
    .........................................................................................................................
    .........................................................................................................................

Treatment after examination:

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certify that the abovementioned has been examined and found fit to pursue for further education.

Signature........................................................

Designation....................................................

Station............................................................

(Official stamp).................................

Date................................................................

**NB**:Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na Serikali.